# Tani 100 za nyama kusafirishwa Misri

**Na MWANDISHI WETU**

SERIKALI kwa kushirikiana na Taasisi ya Huduma za Miradi ya Misri (NSPO), inatarajia kuanza kuuza nyama ya Tanzania nchini humo, kabla ya sikukuu ya Eid al Hajj tani 100 zitasafirishwa.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dodoma na Makamu Mwenyekiti wa NSPO, Meja Jenerali Hossam Nigeda, wakati akizungumza na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega.

Nigeda alisema wamejipanga kuanzisha machinjio ya kisasa hapa nchini, ambayo itawezesha kusafirisha tani 600 ya nyama kila mwezi.

Pia, alisema lengo lao ni kuendelea kuimarisha ushirikiano wa nchi hizo mbili kwa kufungua soko la nyama ya Tanzania nchini Misri ambalo pamoja na mambo mengine, watasafirisha wanyama hai wakiwemo ng'ombe, kondoo na mbuzi 10,000 kila mwezi.

Kwa upande wake Waziri Ulega, alimuhakikishia Meja Jenerali Nigeda, Tanzania ipo tayari kutoa ushirikiano wa kutosha kufanikisha biashara hiyo ianze haraka iwezekanavyo.

Ulega alisema Misri ni miongoni mwa nchi yenye idadi kubwa ya watu barani Afrika, ambayo hawapungui milioni 120, hivyo kufanyika biashara hiyo ni fursa nzuri katika uchumi wa Tanzania.

Aidha, wajumbe wengine waliombatana na Meja Jenerali Nigeda ni Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Taifa ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji, Islam Attia Abdel Hamid, Mwenyekiti wa Huduma za Mifugo, Misri Meja Jenerali Dk. Ihab Saber Youssef na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Masr Trading, Dk. Hatem Ahmed.

Ziara hiyo ni miongoni mwa jitihada za Rais Samia za kufungua milango ya kibiashara nje ya nchi.


## MACHINJIO

**KUANZISHWA**

Alisema wamejipanga kuanzisha machinjio ya kisasa nchini itakayowezesha kusafirisha tani 600 ya nyama kila mwezi.

CamScanner

uzi,
ja,
adi
Dk.
ja,



**MAKAMU** Mwenyekiti wa Taasisi ya Taifa ya Huduma za Miradi (NSPO), Meja Jenerali Hossam Nigeda (kulia), akimkabidhi Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, barua ya mwaliko wa kwenda nchini Misri kuona shughuli za sekta ya mifugo na uvuvi zinavyoendeshwa, Dodoma, jana.

CamScanner

# Nyama ya Tanzania kuanza kuuzwa Misri

Na Mbaraka Kambona

NYAMA ya Tanzania itaanza kuuzwa nchini Misri baada ya ujumbe kutoka nchini humo kukutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega na kumweleza kuwa lengo lao kabla ya Sikukuu ya Eid al Hajj waanze kusafirisha tani 100 za nyama ili kuanza kutangaza soko la Tanzania.

Hayo yalifahamika wakati wa kikao cha "Breakfast Meeting" kilichofanyika jijini Dodoma jana baina ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Ujumbe kutoka nchini Misri ulioongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Taifa ya Huduma za Miradi (NSPO), Meja Jenerali Hossam Nigeda.

Meja Generali, Nigeda alimweleza Waziri Ulega kuwa lengo lao ni kuendelea kuimarisha ushirikiano wa nchi hizo mbili kwa kufungua soko la nyama ya Tanzania nchini Misri.

Pia wamejipanga kuanzisha machinjio ya kisasa hapa nchini ambayo itawawezesha kusafirisha tani 600 ya nyama kila mwezi, kusafirisha wanyama hai wakiwamo ng'ombe, kondoo na mbuzi 10,000 kila mwezi.

Alifafanua kuwa kwa siku za hivi karibuni wapo katika mipango ya kusafirisha tani 100 za nyama kabla ya Sikukuu ya Eid Al Hajj ili kuanza kutangaza soko la nyama ya Tanzania nchini humo.

Misri ni miongoni mwa nchi zenye idadi kubwa ya watu barani Afrika ambao hawapungui milioni 120 na kuwa fursa nzuri ya kibiashara kwa Tanzania hususani biashara ya nyama.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Ulega alimhakikishia Meja Jenerali Nigeda kuwa Tanzania ipo tayari na watawapa ushirikiano wa kutosha ili kufanikisha biashara hiyo iweze kuanza haraka iwezekanavyo.

Wajumbe wengine waliombatana na Meja Jenerali Nigeda ni Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Taifa ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji, Islam Attia Abdel Hamid, Mwenyekiti wa Huduma za Mifugo, Misri, Meja Jenerali, Dk. Ihab Saber Youssef na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Masr Trading, Dk. Hatem Ahmed.

Ziara hiyo ni miongoni mwa jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan za kufungua milango ya kibiashara nje ya nchi.

CamScanner

# Egypt to start importing meat from Tanzania

By Guardian Correspondent

MEAT from Tanzania will be sold in Egypt following talks with a delegation from the North African country with the minister for Livestock and Fisheries, Abdallah Ulega.

THE Egyptian delegation assured the minister that before the Eid el Hajj holiday, they should start importing 100 tonnes of meat.

Ulega made the revelation at a brief breakfast meeting in Dodoma yesterday shortly after meeting the Egyptian delegation that was led by the vice chairman of the country's National Service Projects Organisation (NSPO), Maj. Gen. Hossam Nigeda.

During the discussion, Maj. Gen Nigeda told the minister that their aim is to continue strengthening the existing cooperation between the two countries by opening a meat market in Egypt. He added that they are mobilised to establish a modern abattoir in Tanzania that will enable them to export 600 tonnes of meat each month, including live animals of 10,000 cattle, sheep and goats every month.

He explained that in the coming days they are in plans to import 100 tonnes of meat before the Eid el Hajj holiday in order to start advertising Tanzania meat in Egypt.

Egypt is among African countries with a big population, not less than 120 million hence it will be a good trade opportunity for Tanzania in meat trade.

For his part, Livestock and Fisheries Minister Ulega assured Maj Gen Nigeda that Tanzania is ready and will provide adequate cooperation to make the meat trade a success.

Other members in the Egyptian delegation included the chief executive officer of the National Fisheries and Marine Life Corporation, Islam Attia Abdel Hamid, chairman of Egypt's Livestock Services Maj. Ge Ihab Saber Youssef and the chief executive officer of Trading Company, Dr Hatem Ahmed.

CamScanner

# Tani 100 za nyama kusafirishwa Misri

SERIKALI kwa kushirikiana na Taasisi ya Huduma za Miradi ya Misri (NSPO), inatarajia kuanza kuuza nyama ya Tanzania nchini humo, kabla ya sikukuu ya Eid al Hajj tani ...

>>>INAENDELEA Uk. 6



# Nyama kutoka Tanzania yapata soko, kuanza kuuzwa nchini Misri

**Mwandishi Wetu**, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Dodoma.** Nyama kutoka Tanzania itaanza kuuzwa nchini Misri kabla ya Sikukuu ya Eid al hajj, imeelezwa.

Hayo yalisemwa jana jijini Dodoma wakati ujumbe kutoka nchini humo ulioongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Taifa ya Huduma za Miradi (NSPO), Meja Jenerali Hossam Nigeda ulipokutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega.

Meja Jenerali Nigeda alisema lengo lao ni kuanza kusafirisha tani 100 za nyama kabla ya sikukuu ya Eid, ili kuanza kutangaza soko la nyama kutoka Tanzania.

Mbali ya biashara ya nyama, Nigeda alisema Misri inalenga pia kuendelea kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizo mbili kwa kufungua soko la nyama kutoka Tanzania.

Alisema wamejipanga kuanzisha machinjio ya kisasa hapa nchini ambayo itawawezesha kusafirisha tani 600 za nyama kila mwezi sambamba na kusafirisha wanyama hai wakiwamo ng'ombe, kondoo na mbuzi 10,000 kila mwezi.

> **"Tumejipanga kuanzisha machinjio ya kisasa hapa nchini ambayo itatuwezesha kusafirisha tani 600 za nyama kila mwezi na kusafirisha wanyama hai wakiwamo ng'ombe, kondoo na mbuzi 10,000 kila mwezi."**
> Meja Jenerali Hossam Nigeda

"Misri ni miongoni mwa nchi zenye idadi kubwa ya watu barani Afrika, ikiwa na watu wasiopungua milioni 120, hivyo itakuwa fursa nzuri ya kibiashara kwa Tanzania hususan hii ya nyama," alisema.

Kwa upande wake, Waziri Ulega alimuhakikishia Meja Jenerali Nigeda kuwa Tanzania ipo tayari na itawapa ushirikiano wa kutosha ili kufanikisha biashara hiyo iweze kuanza haraka iwezekanavyo.

"Na hii ziara ni miongoni mwa jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kufungua milango ya kibiashara nje ya nchi," alisema Waziri Ulega.

Wajumbe wengine waliombatana na Meja Jenerali Nigeda ni Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Taifa ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji, Islam Attia Abdel Hamid, Mwenyekiti wa Huduma za Mifugo, Misri, Meja Jenerali, Dk Ihab Saber Youssef na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Masr Trading, Dk Hatem Ahmed.